



Msiingie miji ya wale waliozidhulamu nafsi zao, isipokuwa muwe mnalia

Kutoka kwa Abdallah bin Omari radhi za Allah ziwe juu yao yeye na baba yake, amesema: Tulipita tukiwa pamoja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika Hijiri (miji ya Thamudi), akasema kutuambia Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

"Msiingie miji ya wale waliozidhulamu nafsi zao, isipokuwa muwe mnalia; kwa kutahadhari msijekupatwa na mfano wa yale yaliyowapata" Kisha akampigia kelele mnyama wake akaongeza mwendo mpaka akapapita.

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaari na Muslim]

Alikataza Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipopita katika miji ya Thamudi, kutoingia katika miji ya walioadhibiwa, wale waliozidhulamu nafsi zao au kuiendea miji hiyo, isipokuwa anayeingia kama atakuwa analia kwa kuchukua mazingatio kwao; kwa kuhofia asijekufikwa na mfano wa yale yaliyowafika mionganini mwa adhabu, kisha akampigia kelele mnyama wake akaongeza mbio mpaka akaivuka.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66294>